Barry, A. L. - WHAT ABOUT? THE BIBLE
- *Swahili*

Kuhusu Jambo Gani...

# Biblia

**Daktari A. L. Barry**
**Rais**
**Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri**

Salamu kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo. Biblia inaendelea kuwa kitabu bora zaidi cha wakati wetu kilichopata kuuzwa. Vizazi hata vizazi, Biblia imetoa uvuvio (inspiration), faraja na mwongozo kwa wale waliokwisha kuisoma. Lakini je, Biblia ni kitabu cha uvuvio tu? Ndivyo kilivyo, lakini ni zaidi huo!

Hebu sasa tuchukue muda kiasi kuzihakiki baadhi ya kweli muhimu kuhusu Biblia.

**Biblia ni Nini?**

Neno "Biblia" linatokana na neno la Kiyunani lenye maana ya "kitabu." Hiki "kitabu chema" ni kipi? Jibu la swali hili lina sehemu mbili.

Kwanza, Biblia hasa ni mkusanyiko wa vitabu – 66 kamili – kutoka cha kwanza, Mwanzo, mpaka cha mwisho, Ufunuo. Vitabu hivi huzungumzia miaka elfu kadhaa na viliandikwa ama katika Kiebrania, Kiaramu au Kiyunani. Kuna aina nyingi sana tofauti za maandiko katika Biblia: masimulizi ya kihistoria, unabii, ushairi, hotuba, nyaraka, na kadhalika. Kutokana na mtazamo wa kibinadamu tu, hakuna shaka kwamba, Biblia ni kazi bora sana ya fasihi kuliko zote.

Pili, hili ndilo jibu lililo muhimu sana kwa swali, "Biblia ni nini? Biblia ni Neno la Mungu. Biblia ni mkusanyiko wa mawazo – hata maneno yale yale – ambayo Mungu aliwapatia waandishi wa vitabu vya Biblia. Biblia ni kipawa ambacho Mungu amelipatia kanisa Lake. Si kusanyiko la hekaya na hadithi za kale. Biblia ni njia ya kweli na thabiti ambayo Mungu, Roho Mtakatifu hutumia kulipitisha Neno Lake kwetu siku hizi.

**Tuliipokeaje Biblia?**

Biblia yenyewe huelezea tulivyoipokea. "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki" (2 Tim. 3:16). Kwingineko tunasoma kwamba, "Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Pet. 1:21).

Kwa kuwa watu walijua kwamba, Biblia ilikuwa Neno halisi la Mungu, lililonakiliwa na kunakiliwa tena kwa uangalifu mkubwa na kwa makini kikamilifu, herufi kwa herufi, na neno kwa neno. Ingawa siku hizi hatuna matini halisi tena na ya asili ya Biblia, tunaweza kuwa na hakika kwamba, Roho Mtakatifu amelihifadhi Neno la Mungu kwa ajili yetu. Uchunguzi mwangalifu wa nakala elfu kadhaa za Agano Jipya huonyesha kwamba, ingawa kuna tofauti ndogo kati ya nakala mbalimbali, hakuna mahali ambapo fundisho muhimu la Biblia linahitilafiana.

Biblia zetu za Kiswahili ni tafsiri kutoka kwa lugha za asili. Tunapotumia tafsiri za kutegemewa, tunaweza kuwa na hakika kwamba, tuna Neno halisi la Mungu. Ambalo ni Neno la Mungu katika Kiebrania, Kiaramu au Kiyunani, ndilo lilo hilo pia [Neno la Mungu] katika Kiswahili, au katika lugha nyingine yoyote, mradi tu tafsiri iwe aminifu kwa lugha za asili. Tafsiri za kutegemewa ni pamoja na Union Version [ambayo tunaitumia katika tafsiri zetu] na Habari Njema.

**Kwa Nini Biblia ni Muhimu sana?**

Mtu fulani anaweza kusema, "Biblia ni muhimu kwangu kwa sababu huniambia la kutenda" na mtu mwingine anaweza kusema, "Masimulizi ya zamani hunikumbusha kuhusu utoto wangu" au "Biblia ni mwongozo wa maisha ya kila siku." Majibu haya yote yana ukweli mdogo sana, lakini yanakosa sababu halisi ya umuhimu wa Biblia: Ni asili ya kweli na thabiti ya kumjua Yesu Kristo ni nani na

ambacho amekwisha kukitendea kwa ajili yetu.

Yesu akasema, "Maandiko [Matakatifu] hunishuhudia Mimi (Yohana 5:39). Ujumbe muhimu wa Biblia ni Habari Njema za kazi ya Mungu ili kuupatanisha ulimwengu Naye Mwenyewe kwa njia ya uhai, mauti na kufufuka kwa Yesu. Kote kote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ujumbe mkuu wa Biblia ni maelezo kuhusu namna Mungu alikuja ulimwenguni kuutayarisha ili umpokee Mwanawe na ambalo Mwanawe alilitenda alipokuwa humo. Vile vile yanatuambia namna kanisa liliupokea ujumbe huu wa utukufu wa wokovu, na jinsi ulikua na kuenea kote kote katika ulimwengu tunaoujua. Wakati mmoja, Luther aliilinganisha Biblia na nguo za kitoto alizovikwa Yesu. Hivyo, Biblia inamlenga Kristo.

Bwana wetu Yesu akasema, "Ninyi mkikaa katika Neno Langu, mmekuwa wanafunzi Wangu kweli kweli" (Yohana 8:31). Mamlaka ya Uungu na tumaini la Biblia havitegemei watu aliowatumia Mungu ili kuiandika Biblia, wala katika kuungwa mkono kwa Biblia na kanisa, bali hutegemea hasa ukweli kwamba, ni Neno la Bwana. Tunalijuaje hili? Ukiri huu wa mamlaka kamili ya Biblia ni sehemu hakika ya imani ambayo Mungu hutupatia kama kipawa.

Wanadamu halisi walipatiwa maneno halisi na Mungu ili wayaandike. Ambavyo Bwana wetu Yesu Kristo alikuwa Mungu kweli na mwanadamu kweli, vivyo hivyo Biblia ni Neno la Mungu kwa kweli na hivyo maandiko ya wanadamu. Hata ambavyo Bwana wetu Yesu alivyochukua mwili wa mwanadamu usiokuwa na dhambi wala makosa, ndivyo Mungu alivyowatumia wanadamu ili kutoa ufunuo ulioandikwa juu Yake Mwenyewe ambao hauna makosa. Hivyo, tunaamini kwamba, Biblia haikosei (infallible) wala haina makosa (inerrant).

Biblia ina tofauti kubwa sana ambayo mtu anahitaji kuikumbuka ili aweze kuifahamu bila kukosea: tofauti kati ya Sheria na Injili. Biblia hufunua utakatifu kamili na haki, na matarajio Yake ya ukamilifu. Sheria Yake iliyofupishwa vizuri sana katika Amri Kumi, huzifunua dhambi zetu za kuasi na kutoweza kwetu kujiokoa wenyewe. Injili ndizo Habari Njema za furaha kwamba, Bwana wetu Yesu Kristo ametupatia msamaha kamili wa dhambi zetu kwa njia ya uhai, mauti na kufufuka Kwake kwa ajili yetu. Tofauti sahihi kati ya Sheria na Injili ndiyo msingi wa kuifahamu Biblia sawasawa.

Ujumbe muhimu sana wa Biblia siyo Sheria ya Mungu. Biblia si mkusanyiko tu wa kanuni kwa ajili ya maisha ya kila siku. Biblia siyo tu kitabu kinachojibu kila swali tunaloweza kuwa nalo. Wala ilivyo, Biblia si kitabu kinachoagua kila tukio la mwisho kuhusu siku zijazo. Lililo kuu na fundisho muhimu sana katika Biblia ni Injili, Habari Njema za kipawa cha Mungu cha wokovu kwa njia ya Yesu Kristo. Injili ndiyo ujumbe wenye nguvu sana katika Biblia nzima, kutoka Agano la Kale mpaka Agano jipya. Hivyo, Biblia inailenga Injili.

Tunajua kwamba, Biblia haikutolewa tu kwa ajili ya kutolewa. Hatuokolewi kwa sababu tuna Biblia. Tunaokolewa na Bwana wetu Yesu Kristo, anayefunuliwa katika Biblia. Tunaiamini Biblia kwa sababu ni Neno la Bwana. Tunamwamini [Bwana], na hivyo tunaliamini Neno Lake kuwa kweli. Tunayapokea aliyokwisha kutupatia. Ametupatia Maandiko Matakatifu. Hivyo, Biblia ndiyo msingi na kigezo (touchstone) kwa kila kitu ambacho kanisa huamini, hufundisha, hukiri, na kutenda. Kwa nini? Kwa sababu Biblia ni Neno la Bwana linalovuviwa, linalomlenga Kristo na linaloilenga Injili.

**Tunaitumiaje Biblia?**

Biblia ndiyo msingi kwa huduma ya kanisa. Biblia haikukusudiwa kamwe kujisimamia peke yake au kuwa mbali na jamii ya imani tunayoiita Kanisa la Kikristo. Ni sikitiko wakati watu wengine hufikiria kwamba, wakiisoma tu Biblia, wanaweza kuacha kwenda kanisani. Tunapokea vipawa vya Bwana wetu kwa furaha na hatusemi, "Tunalitaka hili, bali si lile." Ingekuwa upotovu iwapo heshima yetu kuu kwa Maandiko Matakatifu ingetumika kutenganisha Biblia na kanisa. Kanisa ni kusanyiko la watu wa Mungu palipo na Neno la Bwana na Sakaramenti. Maandiko Matakatifu ndiyo ufunuo wa kweli na thabiti wa Neno la Mungu na hivyo yanapasa kusomwa, kuchunguzwa, na kutafakariwa na Wakristo kanisani na nyumbani.

Sisi Walutheri hutambua kwamba, Maandiko Matakatifu lazima yafafanuliwe kufuatana na kweli kuu ya Biblia, Injili, siyo iliyochukuliwa kutoka hapa na pale na kufundishia mambo ambayo yanahitilafiana na Injili. Kwa hiyo, tunakuwa waangalifu katika sarufi na maneno ya Biblia, huku tukitafuta maana inayokusudiwa, ambayo ni maana wazi ya matini (text). Tunatambua kwamba, Mungu, Roho Mtakatifu hufanya kazi kwa njia ya Maandiko Matakatifu ili kufanyiza na kutegemeza kanisa linapokusanyika ambapo Neno huhubiriwa na Sarakramenti kutolewa.

Ambapo Neno la Mungu linahubiriwa, linafundishwa, linachunguzwa, linasomwa, linaarifiwa au kutafakariwa, Roho Mtakatatifu anatenda kazi kuwageuza watu kutoka dhambini na kuwavutia Kwake Kristo kwa ajili ya wokovu wao. Hivyo, tungependa kuwa katika Neno kila siku. Nyumbani tunasoma na kutafakari Neno kwa njia ya sala za faragha na za jamaa. Msingi wa Neno la Mungu kanisani ni nyimbo zetu za dini na liturgia. Wachungaji wetu hutuhubiria katika msingi wa masomo ya Biblia yaliyoteuliwa kwa kila Jumapili katika mwaka wa kanisa. Walimu wetu shuleni huwaongoza watoto wetu katika ujuzi wa kina wa Neno la Mungu. Katika Shule ya Jumapili, watoto hujifunza masimulizi ya Biblia na hivyo, huwa na msingi kwa ajili ya maisha yao. Katika masomo ya Biblia kwa vijana na watu wazima, Maandikoa Matakatifu huchunguzwa kwa njia mbalimbali ili yaweze kutujulisha na kutuelimisha na kutusaidia tufahamu tunavyoishi maisha yetu kama watu wa Mungu.

Maandiko Matakatifu ni kipawa kilichobarikiwa cha namna gani kwetu na kwa watu wote! Kila jambo ambalo Mungu anataka tulijue kumhusu Yeye Mwenyewe linapatikana katika Neno Lake. Kwa njia ya Maandiko Matakatifu, Roho Mtakatifu hufunua kweli kuhusu hali yetu yenye dhambi na habari za furaha za kazi ya Mungu ya kutuokoa kwa njia ya Mwana Wake, Yesu Kristo. Hakika, Neno la Mungu ndilo taa ya miguu yangu na mwanga wa njia yangu (Zab. 119:105). Kwa sababu hiyo tunaomba, "Bwana, tuimarishe katika Neno Lako."

Daktari A. L. Barry
Rais
Kanisa la Kilutheri la Sinodi ya Missouri